

OFISI YA RAIS, TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

SHULE YA SEKONDARI BUJONDE
S.L.P 690
KYELA
SIMU: 0765089745/0785704054
TAREHE.....

FOMU YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 20.....

Kumb. Na. BJND SS/S.3127/JIS/VOL 13/13

JINA LA MWANAFUNZI.....
S.L.P.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA **SEKONDARI BUJONDE**
ILİYOKO WILAYA YA KYELA MKOA WA MBEYA MWAKA 20.....

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga **kidato cha kwanza** katika shule hii mwaka 20..... Muhula wa kwanza masomo yanaanza tarehe Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe..... na mwisho ni tarehendani ya siku saba.

MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya sekondari Bujonde ni ya serikali na ni ya kutwa. Ipo mkoa wa Mbeya wilaya ya Kyela kata ya Bujonde kijiji cha Itope. Ipo umbali wa **km8** kutoka makao makuu ya halmashauri ya Kyela.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

(a) WAVULANA

- i. Suruali mbili { blue bahari na nyeusi }
- ii. Shati mbili za mikono mirefu

(b) WASICHANA

- i. Sketi ya rangi ya machungwa { orange }
- ii. Suruali ya blue bahari
 - Aina ya rangi ya kitambaa cha suruali/sketi imeambatanishwa
 - Rangi ya hijab ifanane na sare za shule

NB: Mshono: sketi linda box urefu wake ufike usawa wa soksi. Suruali ishonwe vizuri ifunike kiatu, si mtindo wa jinsi wala mlegezo

(a) Viatu rangi nyeusi vya kamba

(b) Soksi jozi mbili rangi nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana

(c) Tai rangi inayoendana na suruali kwa wavulana na sketi kwa wasichana

(d)Sare ya michezo kwa shule hii ni :

(i)Truck suit { rangi ya blue bahari }

(ii)Viatu vya michezo jozi moja

(e)T-shirt {rangi ya damu mzee }

NB: (i) Suruali nyeusi/sketi orange zitavaliwa siku ya jumatatu
hadi jumatano

(ii) Suruali blue bahari zitavaliwa siku ya alhamisi na ijumaa

(iii) T-shirt itavaliwa siku ya jumatano/ siku nyingine ya kazi

2.1 Daftari, kalamu na mkebe wa hesabu

2.2 Chakula cha wanafunzi wa kutwa,nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu

2.3Nauli ya wanafunzi wa bweni kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo , godoro na vifaa vya malazi

2.4Mahitaji mengine ya kibinadamu

3.0SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha,inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na OFISI YA Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

- a) Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni [PREPARATION]
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- i) Kutunza mali za umma

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- (a)Wizi
- (b)Uasherati na ushoga
- (c)Ubakaji
- (d)Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile uvutaji bangi, cocaine,mirungi, kubeli na kadhalika
- (e)Kupigana au kupiga
- (f)Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- (g)Kudharau bendera ya taifa
- (h)Kuwa mjamzito/kupata mimba
- (i)Kuoia au kuolewa
- (j)Kutoa mimba
- (k)Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- (l)Kukataa adhabu kwa makusudi
- (m)Kuwa na simu ya mkononi

4.0MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

- a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo , fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

5.0Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
.....

MKUU WA SHULE